

TAARIFA MAALUM KUHUSU HALI YA MAFUTA ZANZIBAR 25/02/2018

Kutokana na Hali ya upungufu wa mafuta iliyotokea kwa takriban wiki mbili zilizopita hasa katika Vituo vya vinamilikiwa na United Petroleum (UP), ZURA imekua ikitoa taarifa mbali mbali kuhusu hali ya Mafuta Nchini kupitia Vyombo mbali mbali ikiwemo Mitandao ya Kijamii, Taarifa hizo zilitolewa mara kwamara kuanzia tarehe 12 hadi 24. Hata hivyo Leo tumeona ipo haja ya kuwaita na kutoa Taarifa hii kupitia Vyombo vya Habari mbali mbali ili kuwaeleza Wananchi hali halisi ya Mafuta Nchini na changamoto zake.

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) imechukua hatua mbali mbali kukabilana na changamoto hiyo, miongoni mwa jitihada zilizofanyika ni pamoja na:-

Serikali kupitia ZURA ilichukua juhudzi za ziada kuhakikisha Meli ya 'United Spirit 1' ya Kampuni ya United Petroleum (UP) inapakia Mafuta ya Petroli Lita 1,820,000 (1400 Metric Tones) katika Bandari ya Dar es salaam. Meli hiyo ilikua katika Foleni ya kusubiria kupakia Mafuta tangu tarehe 18/02/2018, na kufanikiwa kupakia Mafuta hayo Juzi Mchana 23/02/2018 na kufika Zanzibar Usiku wa Siku hiyo. Meli hiyo imefanikiwa kushusha na kusambaza Mafuta hayo Jana 24/02/2018, na Mafuta hayo yanaendelea kusambazwa Vituoni.

Aidha, Meli ya 'MT Ukombozi' ya Kampuni ya GAPCO nayo ilifanikiwa kupakia Mafuta ya Petroli Lita 1,170,000 (900 Metric Tones) na Dizeli Lita 1,080,000 (900 Metric Tones) Jana Jumamosi 24/02/2018 katika Bandari ya Dar es salaam na imefika Zanzibar Jana Usiku, na Mafuta hayo yameanza kushushwa na kusambazwa Vituoni Leo 25/02/2018.

Ni matarajio ya ZURA hali ya upatikanaji wa Mafuta Zanzibar utaendelea kuwa mzuri zaidi baada ya kujiridhisha kuwa Mafuta yaliyopo yameendelea kusambazwa kuanzia Jana Jioni. ZURA inawashukuru sana Wananchi kwa kuwa wastahamilivu, na inawaomba kuendelea kutoa ushirikiano ili kuimarisha huduma za Nishati Nchini.

Pia ZURA inaendelea kusimamia zoezi la usambazaji na uuzwaji wa mafuta vituoni kwa kufuata taratibu za Mamlaka, ili kuhakikisha Mafuta yaliyopo yanauzwa kwa mujibu wa maelekezo ya Mamlaka na kuhakikisha hakuna changamoto yoyote katika upatikanaji wa bidhaa za mafuta nchini.

ZURA inaomba ushirikiano kutoka kwa Wadau wote wa Mafuta na Wananchi katika kukabiliana na changamoto hii.

IMETOLEWA NA KITENGO CHA UHUSIANO (PRU)

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI ZANZIBAR (ZURA)